



GRETCHEN WHITMER  
GOVERNOR

STATE OF MICHIGAN  
OFFICE OF THE GOVERNOR  
LANSING

GARLIN GILCHRIST II  
LT. GOVERNOR

## AGIZO LA UTENDAJI

No. 2020-18

### Vizuizi vilivyoimarishwa kwenye upandaji wa bei

#### Kuondolewa kwa Agizo la Utendaji 2020-8

Virusi vya corona (COVID-19) ni virusi vinavyoathiri mfumo wa upumuaji ambavyo inaweza kusababisha kuwa mahututi au kifo. Husababishwa na aina mpya ya virusi vya corona ambavyo havikuwahi kutambulika kwa wanadamu hapo kabla na ni rahisi kuenea kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Mpaka sasa hakuna chanjo au matibabu ya ugonjwa huu.

Mwezi wa Tatu, tarehe 10, mwaka wa 2020, Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Michigan ilitambua kesi mbili zilizobainika kuwa na maambukizi ya CORONA-19 hapa Michigan. Siku hiyo hiyo, nilitoa agizo la Utendaji 2020-4. Agizo hili lilitangaza hali ya hatari katiko jimbo lote chini ya kifungu cha 1 cha ibara ya 5 cha Katiba ya Michigan ya mwaka 1963, Sheria ya Usimamizi wa Dharura, 1976 PA 390, kama ilivyorekebisha, MCL 30.401-.421, na Nguvu za Dharura za Gavana 1945, 1945 PA 302, kama ilivyorekebisha, MCL 10.31-.33.

Sheria ya Usimamizi wa Dharura inampa gavana nguvu yenye upana na majukumu ya “kukabiliana na hatari serikalini na watu wa serikali husika itakayotokana na janga au dharura”, sheria hiyo ambayo gavana ataitekeleza kupitia “agizo la mtendaji”, matangazo, na maagizo yenye athari na nguvu kisheria.” MCL 30.403(1)-2. Vile vile nguvu ya kisheria ya gavana ya mwaka 1945, inasema kwamba, baada ya kutangaza hali ya dharura, “gavana anaweza kutangaza maagizo, kupitia kanuni na sheria inayofaa kwa ulazima wa kulinda maisha na mali au kuweza kusaidia hali ya dharura kutulia.” MCL 10.31(1).

Kuanzia kutokea kwa dharura hii, imekuwa dhahiri ya kuwa biashara zingine na watu wengine wamekuwa wakiuza vinyago vya uso, sanitaiza za mikono, vifaa vya kusafisha, bidhaa za karatasi, na bidhaa zingine ambazo watu wanaweza kununa kutokana na tishio la COVID-19 kwa bei ya juu isiyo ya haki. Ili kuzuia kuongezeka kwa bei na kusaidia watu wote wa Michigan kupata bidhaa muhimu wakati wa dharura ya COVID-19, ni sahihi na lazima kuweka vikwazo vikali vya muda kuhusu uuzaji wa bidhaa, malighafi, vifaa vya dharura, na vitu vya chakula vya kawaida kwa bei ya juu mno.

Amri ya Utendaji 2020-8 iliweka vizuizi hivyo. Na agizo hili, Agizo la Utendaji 2020-8 limeondolewa. Agizo hili linaweza vizuizi sawa, na baadhi ya marekebisho yaliyofanywa kwa wigo wao.

Kwa kupitia Katiba ya Michigan ya mwaka 1963 na sheria ya Michigan, ninaagiza yafuatayo:

1. Kuanzia sasa na kuendelea hadi Aprili 17, 2020 saa 11:59:00, ikiwa mtu amepata bidhaa yoyote kutoka kwa muuzaji, mtu huyo hafai kuuza tena bidhaa hiyo katika jimbo hili kwa bei ambayo ni ya juu zaidi ya bei ya aliyonunulia.
2. Kuanzia sasa na kuendelea hadi Aprili 17, 2020 saa 11:59:00, mtu asitoe kwa nia ya kuuza au kuuza bidhaa yoyote katika jimbo hili kwa bei ambayo ni zaidi ya asilimia 20 kuliko mtu alivyopendekeza au chaji kutokana na bidhaa hiyo siku ianzapo Machi 9, 2020, isipokuwa mtu huyo aonyeshe kwamba ongezeko la bei linasababishwa na kuongezeka kwa gharama ya kuleta bidhaa sokoni au kwa punguzo la lisilo la kawaida ianzapo Machi 9, 2020.
3. Kwa madhumuni ya agizo hili:
  - a. "Mtu" inamaanisha mtu binafsi, biashara, au chombo kingine cha kisheria. "
  - b. "Bidhaa" inamaanisha kitu bidhaa yoyote, au malighafi, au ununuzi wa chakula kwa bei inayotakiwa sokoni chini ya \$ 1,000.00, au usambazaji wowote wa dharura.
4. Agizo hili halizui au kudhoofisha uwezo wa wakili mkuu wa kuchunguza, kuamua, au kuweka dhima chini ya sheria ya ulinzi mnunuzi ya Michigan, ya mwaka 1976 PA 331, kama ilivyorekebisha, MCL 445.901-.922, au sheria nyingine yoyote ya jimbo hili.
5. Kulingana na MCL 10.33 na MCL 30.405 (3), ukiukaji wa makusudi wa amri hii ni uvunjaji wa sheria.
6. Agizo la Utendaji 2020-8 limeondolewa.

Imetolewa kwa saini ya mkono wangu na Muhuri Mkubwa wa Michigan

Tarehe: Machi 20, 2020

Wakati: 3:37 jioni



GRETCHEN WHITMER  
GAVANA

Na Gavana:

---

KATIBU WA SERIKALI